

## **Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)**

### **BUNGE LA TANZANIA**

---

### **MAJADILIANO YA BUNGE**

---

### **MKUTANO WA ISHIRINI**

**Kikao cha Kwanza – Tarehe 7 Juni, 2005.**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

### **D U A**

*Spika (Mhe. Pius Msekwa) Alisoma Dua*

### **TAARIFA YA SPIKA**

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, ninazo taarifa tatu zifuatazo:- Taarifa ya kwanza ni ya huzuni, inahusu msiba tulioupata sisi kama Bunge kwa kufiwa na Mbunge mwenzetu Mbunge wa Kilombero, Mheshimiwa Abu Towagale Kiwanga, aliyefariki dunia katikati hapa tangu tulipokutana mara ya pili, kuachana mara ya mwisho baina ya wakati huo na leo tumeshampoteza Mbunge mwenzetu. Kwa hiyo, kwa taratibu zetu za kawaida naomba sasa tusimame kwa dakika moja ili tuiombe roho ya Marehemu Mwenyezi Mungu aiweke mahali pema Peponi. *Amin.*

*(Hapa Wabunge walisimama kimya kwa dakika moja kuomboleza kifo cha Mbunge aliyefariki)*

**SPIKA:** Tunaweza kukaa.

Taarifa ya pili inahusu Miswada mitano ambayo tuliipitisha katika Bunge hili katika Mkutano wetu wa mwezi Aprili, 2005 na taarifa ni kwamba yote imeshapata kibali cha Mheshimiwa Rais na sasa ni Sheria za Nchi. *(Makofi)*

Taarifa ya tatu na ya mwisho, inahusu ratiba ya leo. Kama mnavyoona kwenye *Order Paper*, tumeweka Muswada wa kujadiliwa asubuhi hii, lakini taarifa ni kwamba Kamati iliyopelekewa Muswada huu haikuweza kumaliza kushughulikia na Mwenyekiti aliniarifu kwamba wangependa Kamati ikutanishwe na Tume ya Huduma za Bunge ili waweze kupitia masuala fulani yaliyomo katika Muswada ule kwa pamoja. Kwa hiyo, tutakapomaliza kipindi cha maswali asubuhi hii na pengine hii inawafaa na Watanzania wanaotusikiliza kupitia Vyombo vya Habari kwamba leo Bunge litaahirishwa mara baada ya maswali kwa sababu kazi nyingine bado ipo kwenye Kamati na itakuja Bungeni hapo itakapokuwa tayari. Kwa hiyo, baada ya maswali hakutakuwa tena na matangazo kutoka kwenye Ukumbi wa Bunge kwa sababu Bunge litakuwa linaahirishwa.

## HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa mezani na:-

### WAZIRI MKUU:

Mheshimiwa Spika, kabla sijawasilisha nakala za matoleo ya Gazeti la Serikali naomba niseme maneno mawili, matatu. La kwanza, napenda niungane na Waheshimiwa Wabunge wote kutoa pole kwa familia ya mwenzetu ambaye ametangulia mbele ya haki aliyekuwa Mbunge wa Kilombero Mheshimiwa Abu Towagale Kiwanga. Napenda kuwapa pole na wananchi wa Kilombero pia kwa kumpoteza Mbunge wao. Mwenyezi Mungu aiweke roho ya Marehemu mahali pema Peponi. *Amin.*

*(Hapa Mheshimiwa Jakaya M. Kikwete aliingia ndani ya Ukumbi wa Bunge na kushangiliwa kwa vijifo na nderemo)*

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, la pili wakati nilipokuwa nikiahirisha Mkutano wa Kumi na Tisa niliwataja Waheshimiwa Augustine Lyatonga Mrema wa *TLP* na Mheshimiwa Profesa Ibrahim Lipumba wa *CUF* kama ambao walikuwa wameteuliwa na Vyama vyao kugombea nafasi ya Urais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na pia nilieleza kwamba Chama cha Mapinduzi kilikuwa katika mchakato wa mikutano mbalimbali ili kupata mgombea wake. Napenda sasa kwanza tukipongeze Chama cha Mapinduzi kwa kufikia mfumo wa demokrasia.

Mheshimiwa Spika, napenda kwa niaba yenu wote kukipongeza Chama cha Mapinduzi na kumpongeza Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kuteuliwa kuwa ndio mgombea rasmi wa nafasi ya Rais wa Jamhuri wa Muungano wa Tanzania kupita Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Katika Kikao hicho pia Mheshimiwa Amani Abeid Karume, aliteuliwa kuwa mgombea wa nafasi ya Rais wa Zanzibar kwa tiketi ya Chama cha Mapinduzi. Kwa niaba yenu napenda kumpongeza sana Mheshimiwa Amani Abeid Karume, kwa uteuzi huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, pia alimpendekeza mgombea mwenza Ndugu yetu Mheshimiwa Dr. Ali Mohamed Shein na yeye napenda kumpongeza sana. *(Makofi)*

Ninaviambia pia Vyama vile ambavyo bado havijapata Wagombea na bado wana nia hiyo, basi wakazane. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo haya, sasa naomba kuwasilisha nakala za matoleo yote ya Gazeti la Serikali yaliyochapishwa tangu Kikao cha mwisho cha Mkutano wa Bunge uliopita hadi leo. Naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

## **MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:**

Hati ya Dharura Kuhusu Muswada wa Sheria ya Kufanya Marekebisho katika Sheria Mbalimbali (*Certificate of Urgency in Respect of The Bill Entitled The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No.2) Bill, 2005.*)

### **MASWALI NA MAJIBU**

Na.1

#### **Siku ya Uchaguzi Nchini**

**MHE. PETER KABISA** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali kupitia Tume ya Uchaguzi inaheshimu Katiba ya Nchi kwa kutoingilia imani ndani ya madhehebu mbalimbali ya wananchi wa Tanzania:-

(a) Je, Serikali iko tayari kuishawishi Tume ya Taifa ya Uchaguzi ili kubadilisha siku na tarehe ya kupiga kura katika Uchaguzi Mkuu kuanzia uchaguzi wa mwaka huu ili iwe siku ambayo haiingilii siku za mapumziko ya waumini wa dini zote yaani Ijumaa, Jumamosi na Jumapili? Badala yake chaguzi zote na hata zile za Serikali za Mitaa zifanyike katika siku za kawaida kama wanavyofanya wenzetu wa Ghana, Burundi, Zimbabwe na Uingereza?

(b) Kwa kuwa mwaka huu hakutakuwa na zoezi la kuandikisha wapigakura kwa sababu tayari tuna daftari la Wapigakura:- Je, kwa nini Uchaguzi usifanyike siku ya kawaida kama vile Jumatano ya mwisho wa mwezi Oktoba, 2005?

(c) Kwa kuwa hivi sasa kuna daftari la kudumu la Wapigakura hivyo uandikishaji wa shahada za wapiga kura hautakuwepo:- Je, Tume ya Taifa ya Uchaguzi inaweza kufupisha kipindi cha Kampeni miezi miwili hadi mwezi mmoja au majuma matatu?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. MUHAMMED SEIF KHATIB)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Peter Kabisa, naomba kutoa maelezo machache ya utangulizi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ratiba ya Uchaguzi Mkuu hupangwa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi kwa kuzingatia Sheria ya Uchaguzi kifungu cha 37(1)(a) kinachoitaka Tume kupanga siku ya uteuzi wa Wagombea sio chini ya siku tano na si zaidi ya siku 25 tokea kuvunjwa Bunge. Aidha, mara baada ya uteuzi wa Wagombea, Tume inatakiwa kupanga siku ya kupiga kura sio chini ya siku 90 baada ya uteuzi wa Wagombea.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, sasa naomba kujibu swali la Mheshimiwa Peter Kabisa, Mbunge wa Kinondoni, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, siku ya Jumapili ya mwisho wa mwezi Oktoba ndiyo imekuwa ikitumika kwa ajili ya kupiga kura hapa Tanzania. Hali hiyo imekuwa ni mazoezi na uzoefu mzuri tokea tulipokuwa na mfumo wa Chama kimoja cha siasa hadi sasa katika mfumo wetu huu wa Demokrasia ya Vyama Vingi vya Siasa na hakuna malalamiko yaliyotolewa na wananchi.

(b) Mheshimiwa Spika, kutumika kwa siku ya Jumapili ambayo ni siku ya mapumziko inawezesha watu wote kuwa huru kwenda Vituoni kwa wakati unaofaa kupiga kura, muda ambao umepangwa kuwa wa saa kumi. Kuwepo kwa Daftari la Kudumu la Wapigakura kutaleta mabadiliko madogo sana ya siku ya upigaji kura kwani itahitajika kila mpigakura kuthibitishwa kuwemo ndani ya daftari hilo ndipo aruhusiwe kupiga kura.

(c) Mheshimiwa Spika, Tume imepanga miezi miwili kwa madhumuni ya kuwepo kwa muda wa kutosha kwa ajili ya Wagombea na Vyama vya Siasa kufanya Kampeni. Hali kadhalika, kuwezesha kukamilisha taratibu zinazohitajika kwa ajili ya siku ya kupiga kura. Taratibu hizo muhimu ni pamoja na hizi zifuatazo:-

(i) Kupokea na kushughulikia pingamizi dhidi ya uteuzi wa Wagombea Urais, Ubunge na Udiwani.

(ii) Kupokea na kushughulikia rufaa dhidi ya uteuzi wa Wagombea Ubunge na Udiwani, jambo ambalo ni muhimu sana katika kufahamu Wagombea halali kabla ya kuandaa karatasi za kura.

(iii) Kuandaa na kuchapisha karatasi za kura kwa ajili ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani.

Mheshimiwa Spika, Uchaguzi kufanyika kwa ufanisi ambayo ndiyo azma yetu hutegemea sana kukamilika vizuri kwa shughuli nilizoziainisha. Haitakuwa vyema kwa wakati huu kuishauri Tume kupunguza muda wa Kampeni kuwa mwezi mmoja au majuma matatu.

**MHE. PETER KABISA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa maelezo ya Mheshimiwa Waziri ambayo kwa kweli hayaniridhishi. Lakini nina swali moja la nyongeza. Katika swali langu nilisema kwamba Serikali ihakikishe kwamba haimuingilii mwananchi kwenye dini yake kwa maana iwe ni Muislamu na Mkristo na si kwamba Waislam na Wakristo wanazithamini sana siku za Ijumaa, Jumamosi na Jumapili.

Kwa hiyo, nilikuwa nimeomba kwamba hizi siku zitengwe kwa madhumuni hayo ya waumini kushughulikia mambo ya dini yao na siku maalum ya uchaguzi iwe ni siku ambayo siyo ya kuabudu kwa maana Ijumaa, Jumamosi na Jumapili.

Mheshimiwa Spika, lakini pia napenda kuongeza kwamba si kweli kwamba ukiacha siku ya Jumapili wananchi wanapata nafasi ya kupiga kura wakati wanavyotaka wenyewe. Wengi wanashindwa kupiga kura kwa sababu wanakuwa wako kwenye mambo ya dini zao. Kwanza bado naomba kwamba Serikali ijaribu kutafuta huo ufumbuzi wa kuhakikisha kwamba siku ya kupiga kura inakuwa ni siku ambayo inakuwa siyo siku ya kuabudu. Ahsante.

**SPIKA:** Naona Mheshimiwa umetoa ombi tu hukuuliza swali. Basi Serikali italifikiria kwa wakati wake.

**MHE. YAHYA KASSIM ISSA:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa mnamo mwezi wa Oktoba utakuwa ni mwezi wa Ramadhani ambao ndio siku za kupiga kura na kwa kuwa mwezi wa Ramadhani Waislam wote nyakati kufika Magharibi kina mama wana shughuli maalum ambayo imewawia vigumu kuweza kushughulika na harakati hizo. Je, huoni kwamba ni vizuri badala ya mwezi wa kumi uchaguzi huo kufanya mwezi wa tisa kabla ya mwezi wa Ramadhani?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. MUHAMMED SEIF KHATIB):** Mheshimiwa Spika, Serikali haiingilii sana mambo ya dini zote, lakini tarehe ya Oktoba ndio siku ambayo kwa mujibu wa Katiba ndio siku ya kupiga kura na Waislam wanaweza yote mawili wakafanya wakafunga na kupiga kura. Kwa sababu uchaguzi unakuwa kila baada ya miaka mitano, Ramadhani kila mwaka, kwa hiyo bado nafasi ipo kubwa ya Waheshimiwa Waislam kufunga na kupiga kura, na wala si dhambi kwa dini ya kiislam kupiga kura mwezi wa Ramadhani.

**MHE. ISMAIL J. R. IWVATTA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kunipatia nafasi niulize swali la nyongeza. Kwa kuwa katika zoezi la kuhakiki Daftari la Wapigakura, uhakiki ulifanyika katika ngazi ya Kata. Kuna baadhi ya wananchi katika Vijiji ambao ni mbali kwenda katika Makao Makuu ya Kata hawakupata nafasi ya kwenda kuhakiki.

Je, ikitokea baadhi ya Wapigakura kukawa na hitilafu ya majina yao katika Daftari la Kupiga kura itakuwaje? Watapoteza haki ya kupiga kura?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. MUHAMMED SEIF KHATIB):** Mheshimiwa Spika, Tume ya Uchaguzi imeweka muda maalum kwa Wapigakura kwenda kuchunguza majina yao na kuweka pingamizi na Vituo vimetajwa katika kila eneo. Kwa hivyo, mtu ambaye hakwenda kwa wakati unaofaa, basi hawezi tena kupiga kura mpaka kipindi cha miaka mitano ijayo.

Na. 2

### **Viongozi Waliotembelea Mkoa wa Lindi**

**MHE. OMAR S. CHUBI** aliuliza:-

(a) Je, ni viongozi wangapi wa Kitaifa pamoja na Mawaziri wametembelea Mkoa wa Lindi, tangu mwaka 2000 – Desemba 2004?

(b) Je, Serikali haioni kuwa Mawaziri kupendelea kutembelea Mikoa fulani na kuiacha mingine ni kuwanyima haki wananchi wengine kwa sababu kule ambako Mawaziri hupendelea kutembelea kuna miradi mingi sana ya maendeleo?

(c) Je, ni nani anawajibika kuwahamasisha Mawaziri kutembelea Mikoa?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Omar Said Chubi, Mbunge wa Kilwa Kaskazini, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, tangu mwaka 2000 hadi Desemba 2004 Viongozi wote wa Kitaifa waliutembelea Mkoa wa Lindi. Viongozi hawa ni Mheshimiwa Rais, Mheshimiwa Makamu wa Rais, Mheshimiwa Waziri Mkuu na Mheshimiwa Rais Mstaafu Alli Hassan Mwinyi.

Vile vile, Viongozi 24 ambao ni Mawaziri na Naibu Mawaziri wamefanya ziara Mkoa wa Lindi kwa kipindi hicho na baadhi yao wametembelea Mkoa huo zaidi ya mara moja na hivyo kufanya jumla ya ziara 49 za Viongozi hao katika Mkoa wa Lindi.

Mheshimiwa Spika, maelezo niliyoyatoa katika kujibu sehemu (a) ya swali la Mheshimiwa Omar Said Chubi ni kielelezo cha kutosha kinachodhihirisha jinsi Viongozi wa ngazi za juu wa Kitaifa pamoja na Waheshimiwa Mawaziri na Naibu Mawaziri wanavyotekeleza jukumu lao la kutembelea wananchi Mikoani kwa madhumuni ya kuangalia shughuli zao mbalimbali za maendeleo bila upendeleo. Viongozi hawa hawatembelei zaidi baadhi ya Mikoa kuliko mingine kwa sababu Mikoa hiyo kuna miradi mingi ya maendeleo.

Ninaelewa shauku waliyonayo wananchi wa Lindi ya kutaka Viongozi wawatembelee hata ikiwezekana kila siku, lakini kutokana na hali halisi hili haliwezekani. Tanzania ni nchi kubwa yenye Mikoa 26. Isitoshe Viongozi hawa wanayo majukumu ya kiofisi ya kila siku ndani na nje ya nchi jambo linalowapunguzia sana muda wao wa kutekeleza majukumu mengine kama ya kutembelea Mikoa mara nyingi zaidi kuliko ilivyo hivi sasa.

(b) Mheshimiwa Spika, naomba kumkumbusha Mheshimiwa Mbunge kwamba kila Mkoa una Mkuu wa Mkoa na kila Wilaya ina Mkuu wa Wilaya. Hawa ni Viongozi wanaomwakilisha Rais na Baraza lake lote la Mawaziri katika maeneo yao na wanafanya kazi kubwa na nzuri ya kuwatembelea Wananchi wao mara kwa mara kuhimiza shughuli za maendeleo. Naomba tushirikiane nao hasa Viongozi wa ngazi za juu wa Kitaifa na Mawaziri wanapokosa nafasi ya kutembelea Mikoa.

(c) Mheshimiwa Spika, kama nilivyoieleza hapo awali kutembelea Mikoa ni sehemu ya majukumu ya Viongozi wa ngazi za juu wa Kitaifa na Mawaziri. Hakuna mtu anayewajibika kuwahamasisha wala Viongozi hawa kutembelea Mikoa. Ndiyo maana viongozi 24 wameweza kutembelea Mkoa wa Lindi peke yake kati ya mwaka 2000 na 2004 kama sehemu ya kazi zao na kwa kuzingatia nafasi na muda uliopatikana.

**MHE. OMAR S. CHUBI:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri, naomba niulize swali moja tu la nyongeza. Pamoja na kwamba viongozi hao wametembea zaidi ya 26, lakini kwa masikitiko kutokana na miundombinu ya wakati huo Viongozi huishia Wilayani na Mikoani. Lakini je, hizo ni sehemu ambazo kuna walengwa kwa maana yake watu wengi wenye shauku ya kuona viongozi wao wako Vijijini?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, ziara zote za Viongozi wa Kitaifa pamoja na Baraza la Mawaziri na Naibu Mawaziri zianaandaliwa na Mikoa na Wilaya kwa kushirikiana na Viongozi ndani ya Wilaya au Mikoa hiyo wakiwemo Waheshimiwa Wabunge. Kwa hiyo, unapoonza Kiongozi hakwenda eneo moja au lingine, basi ni kutokana na mazingira halisi ambayo yako katika Mkoa au Wilaya hiyo.

Lakini naomba niongezee tu kwamba siwezi nikasema si kweli, lakini naomba niseme kwa hakika kabisa Viongozi hawa wanapofanya ziara Mikoani na Wilayani wanatumia fursa hiyo kutembelea maeneo mengi kabisa ndani ya Vijiji mbalimbali katika Wilaya na Mikoa inayohusika.

**MHE. DR. CHRISANT M. MZINDAKAYA:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa ni kweli kwamba uko umuhimu na mara nyingi Viongozi wa Kitaifa, Mawaziri wanapotembelea Mikoa mbalimbali wanajifunza na kujua hali halisi ya Wizara zinazowahusu:- Je, Waziri anaweza akatueleza ni kwa nini katika kipindi cha miaka mitano iliyopita Mkoa wa Rukwa umepata Mawaziri wasiozidi saba?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, inawezekana maana sina takwimu za haraka haraka. Ningekuwa nimepata muda ninge-*crosscheck* nione kama ni kweli au si kweli. Lakini naomba niamini tu kwamba alilolisema Mheshimiwa Dr. Chrisant Mzindakaya, ni la kweli.

Mheshimiwa Spika, ninachoweza kusema tu ni kwamba kwa upande inategemea vile vile *initiative* ya Mikoa husika katika kujaribu kuomba viongozi mbalimbali kutembelea maeneo mbalimbali kutembelea maeneo hayo. Lakini upande wa pili inategemea na shughuli ambazo ziko katika Mkoa huo ambazo ndio zinafanya uongozi uende kutembelea maeneo hayo. Kwa hiyo, kwa kweli inabidi wote tushirikiane katika kujaribu kuona ni viongozi gani tunataka waje na kwa wakati gani.

**Magari kwa Wakuu wa Wilaya**

**MHE. MHE KHADIJA SALEH NGOZI (k.n.y. MHE. DR. ZAINAB A. GAMA)** aliuliza:-

(a) Je, ni Wakuu wa Wilaya wangapi Tanzania wasio na magari ya Serikali kwa ajili ya shughuli zao?

(b) Kama wapo baadhi ya Wakuu wa Wilaya wasio na magari:- Je, hali hiyo inaathiri kwa kiasi gani utendaji kazi wao?

(c) Kwa wale Wakuu wa Wilaya wanaotumia magari ya Halmashauri kwa kutokana na magari yao:- Je, shughuli za Halmashauri husika na hasa zile zisizo na mapato makubwa zinaathirika kwa kiasi gani?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Zainab A. Gama, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba hakuna Wakuu wa Wilaya wasio na magari ila ufanisi na hali ya magari haya inatofautiana na kutoka Wilaya moja hadi nyingine. Hata hivyo, magari yote ya Wakuu wa Wilaya yamenunuliwa mwaka 1999 na yana zaidi ya miaka mitano. Kwa kuzingatia ukubwa wa maeneo ya Wilaya zetu na pia ubovu wa barabara ni dhahiri kuwa magari mengi ya Wakuu hawa yamechakaa sana. Kwa kutambua hili Serikali imetenga kiasi cha Shilingi milioni 1.89 katika Bajeti yake ya mwaka 2005/2006 kwa ajili ya kununua magari ya Wakuu wa Wilaya.

(b) Mheshimiwa Spika, kama nilivyokueleza hapo juu hali ya magari ya Wakuu wa Wilaya si ya kuridhisha na ni kweli kwamba kazi nyingi za Wakuu wa Wilaya ni za nje ya Ofisi zao hivyo iwapo magari yao hayafanyi kazi kwa ufanisi yataathiri utendaji wao wa kazi kwa kiasi fulani. Hata hivyo, pamoja na hali hiyo, napenda kuchukua nafasi hii kuwapongeza Wakuu wa Wilaya wote kwa kutenda kazi zao kwa mafanikio makubwa licha ya matatizo yaliyopo ya magari.

(c) Mheshimiwa Spika, Ofisi yangu haina taarifa rasmi kuwa kuna Mkuu wa Wilaya ambaye anatumia gari la Halmashauri kama mbadala wa gari lake la kazi. Ninachoweza kueleza hapa ni kwamba Ofisi za Serikali katika ngazi zote ikiwa ni pamoja na Ofisi za Wakuu wa Wilaya na Halmashauri zinafanya kazi kwa ushirikiano wa karibu sana. Wakuu wa Wilaya ndiyo wanaosaidiana na Halmashauri kusimamia na kutekeleza shughuli mbalimbali za maendeleo. Kwa kuzingatia kwamba Mkuu wa



Wilaya analo gari moja tu haishangazi katika mazingira kama haya ya ushirikiano, Mkuu wa Wilaya anaweza kabisa kutumia gari la Halmashauri wakati gari lake linapokuwa limeharibika au liko katika matengenezo.

Mheshimiwa Spika, naomba kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba tatizo la ubovu wa magari ya Wakuu wa Wilaya tayari linashughulikiwa kati ya Ofisi yangu na Wizara yangu na Wizara ya Fedha kwa madhumuni ya kuongeza ufanisi katika Wilaya zetu zote.

Na. 4

### **Kuzidisha Abiria Katika Mabasi**

**MHE. DR AMANI W. A. KABOUROU (k.n.y. MHE. ASHA A. NGEDE)**  
aliuliza:-

Kwa kuwa, mabasi yanayochukua abiria yanajaza abiria kuliko uwezo wa gari na kinyume na utaratibu na pindi askari wanapokutana na mabasi yenye kuzidisha abiria kwa hali hiyo kuwaamuru madereva walipe faini, lakini jambo la kushangaza ni kwamba, wale abiria waliozidi bado wanaachiwa kuendelea na safari hali wamesimama ndani ya mabasi hayo:-

- (a) Je, hiyo faini inayolipwa inamaanisha nini kama siyo kuhalalisha kosa?
- (b) Je, Serikali haioni kuwa ikiwa itawateremsha waliozidi na kuliruhusu gari kuendelea na safari itakuwa fundisho kwa abiria wanaopanda gari hali likiwa tayari limejaa na kwa kufanya hivyo pia kutapunguza idadi ya watu wanaokufa au kujeruhiwa vibaya endapo ikitokea ajali?

**NAIBU WAZIRI MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Asha Ndege, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, faini anayotozwa mwenye basi aliyezidisha abiria haihalalishi kosa, bali ni adhabu kwa mhusika kwa kuvunja Sheria ya Usalama Barabarani Na.30 ya mwaka 1973. Faini hii inaweza kutozwa papo kwa papo iwapo mhusika amekubali kosa. Lakini iwapo atakataa kukiri kosa, hupelekwa Mahakamani na huko huadhibiwa. Hivyo, faini hii hutozwa ili kumwadhibu mwenye gari lililofanya kosa na sio vinginevyo.

(b) Mheshimiwa Spika, Sheria hii kama ilivyo hivi sasa, inamtia hatiani mwenye basi na kumwacha abiria aliyezidi ndani ya basi kwamba hana hatia. Kutokana na upungufu huu, hivi sasa Serikali inaandaa marekebisho ya sheria hii ili iwabane na kuwatia hatiani pia abiria wanaokubali kupanda basi ambalo tayari limejaa.

Wakati tunasubiri marekebisho hayo ya Sheria, Serikali imekuwa inatoa elimu kwa abiria kuacha kupanda magari yaliyojaa, kwani basi linapopata ajali, abiria waliosimama ndiyo hupata maafa makubwa zaidi. Vile vile, Askari wa Trafiki wamepewa uwezo wa kuwateremsha abiria waliozidi kutegemea na hali halisi ya kila tukio.

Mheshimiwa Spika, napenda kurudia kutoa wito kwa wananchi waanze kujenga tabia ya kutokupanda mabasi yaliyojaa kwa usalama wa maisha yao na abiria wengine.

Na. 5

### **Upigaji Saluti**

**MHE. SALOME J. MBATIA** aliuliza:-

- (a) Je, kitendo cha kupiga Saluti kinachofanyika na Askari maana yake ni nini?
- (b) Je, ni Askari wa *rank* gani ambao hupigiwa Saluti?
- (c) Je, ni Maafisa Viongozi wa *rank* gani uraiani katika mihimili ya *Executive*, *Judiciary* na *Legislative* wanaostahili kupigiwa Saluti?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Salome Joseph Mbatia, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, kitendo cha kupiga Saluti kinachofanywa na Askari maana yake ni kutoa salaam kwa ishara yenye kuonyesha heshima. Aidha, Saluti pia ni njia mojawapo ya kuonyesha heshima na utii kwa Kiongozi Mkuu kwenye Asasi za Kijeshi.

(b) Mheshimiwa Spika, Maofisa wote ni lazima wapige Saluti kwa Viongozi wao wenye vyeo zaidi. Askari wote wa ngazi za chini (*Rank and File*) nao wanalazimika kuwapigia Saluti Viongozi wao Wakuu, yaani Maofisa pamoja na Wakaguzi (*Inspectors*).

(c) Kwa mujibu wa Kanuni za Jeshi la Polisi (*PGO*) Na.102 Viongozi wengine katika Mihimili ya Utawala (*Executive*), Mahakimu (*Judiciary*) na Bunge (*Legislative*) wanaostahili kupigiwa Saluti ni:-

- Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambaye ndiye Amiri Jeshi Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi na Usalama.
- Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

- Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.
- Mheshimiwa Waziri Mkuu.
- Mheshimiwa Waziri Kiongozi wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.
- Waheshimiwa Mawaziri na Manaibu Waziri wa Serikali zote mbili.
- Mheshimiwa Spika wa Bunge la Muungano.
- Mheshimiwa Spika wa Baraza la Wawakilishi – Zanzibar.
- MMheshimiwa Jaji Mkuu.
- Mheshimiwa Jaji Kiongozi.
- Waheshimiwa Majaji wote.
- Waheshimiwa Wabunge wote wanapokuwa katika eneo la Bunge na wanapokuwa kwenye Majimbo yao. Nitarudia. (*Kicheko*)
- Waheshimiwa Wabunge wote wanapokuwa katika eneo la Bunge na wanapokuwa kwenye Majimbo yao.
- Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi wote wanapokuwa katika eneo la Baraza na wanapokuwa katika Majimbo yao.
- Wakuu wa Mikoa wakiwa kwenye Mikoa yao. Wakuu wa Wilaya wakiwa katika Wilaya zao.
- Mahakimu wa Mikoa na Wilaya wanapigiwa Saluti na Askari wenye Cheo kuanzia Mkaguzi (*Inspector*) na Askari wa *Rank and file* wakiwa katika eneo la Mahakama.

**MHE. IBRAHIM W. MARWA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi niulize swali dogo la nyongeza:-

Kwa kuwa katika jibu la msingi, Mheshimiwa Naibu Waziri amezungumzia suala la heshima kwa Viongozi, ni kwa nini inapokuja kwa Wabunge iwe ni ndani ya Majimbo yao na si sehemu nyingine yoyote?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli katika jibu langu la msingi nimesema Wabunge wanapigiwa Saluti wakiwa kwanza kwenye eneo la Bunge na wanapokuwa kwenye maeneo yao ya kazi ya Majimbo na si Wabunge tu peke yao, nimesema vile vile hata Wakuu wa Mikoa wakiwa katika Mikoa

yao ya kazi, wale walio chini yake pale wote lazima wamtii na kumheshimu, nimesema Wakuu wa Wilaya, akiwa katika Wilaya yake walioko chini yake katika Mamlaka yake lazima wamtii na kumheshimu na vilevile Mahakimu wa Mkoa na Wilaya wakiwa katika eneo la kazi pale, lazima wale walioko chini yake wamheshimu na wamtii.

**MHE. HAJI JUMA SEREWEJI:** Mheshimiwa Spika, naomba kuuliza swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa Mbunge yoyote wa Tanzania anaitwa Mbunge wa Jamhuri ya Muungano na anapigiwa Saluti katika Jimbo lake na akiwa sehemu ya Bunge:- Je, haionekani kwamba amepunguziwa uwezo na inakuwa kama akiwa yuko nje ya maeneo hayo ya kupigiwa Saluti, inaonekana kwamba ubingwa wake haupo? (*Kicheko/ Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI:** Mheshimiwa Spika, kwa kweli sikubaliani na Mheshimiwa Mbunge kwamba Mbunge kwa mfano Sereweji akija kule kwangu Manyoni kwa shughuli zake, maana kule si Jimbo lake, amekuja tu kwa shughuli nyingine labda kunisalimia, sasa Askari wa kule Manyoni wakimpita bila kumpigia Saluti labda pengine hawamfahamu maana wanayemjua ni mimi. (*Kicheko*)

**WABUNGE FULANI:** Hata!

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI:** Mheshimiwa Spika, wakimpita sasa wala kwa kweli hawajampunguzia heshima na uzito wa Ubunge wake. (*Kicheko*)

**MHE. ELIACHIM J. SIMPASA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi. Mkuu wa Mkoa anapopita kwenye Mkoa mwingine ninavyofahamu, huwa anateremsha bendera yake, sidhani kama wanatembea Mkoa yote wanapeperusha bendera ya Mkuu wa Mkoa. Lakini Mbunge anapotembea anaruhusiwa kwa Sheria tuliyopitisha hapa Bungeni kupeperusha bendera nchi nzima. Je, kwa heshima ya Bendera hiyo, anapopita pale kwa nini hawezi kupigiwa Saluti, kwa heshima ya bendera? Au bendera hii haina heshima?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI:** Mheshimiwa Spika, shughuli hizi zinakwenda kwa mujibu wa Sheria na ziko Sheria mbili tofauti, iko Sheria ya Bendera na taratibu zake na iko Sheria ya Saluti. Sasa swali la msingi lilihusu Saluti na nikataja kifungu cha Sheria cha Saluti nilikitaja kwamba kiko katika *PGO* Na.102. Sheria hii ndiyo imeorodhesha mlolongo nani apigiwe na wapi. Sheria ya Bendera nayo ipo na ina utaratibu wake. Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Simpasa tusichanganye haya mambo mawili kwa sababu yanatawaliwa na Sheria mbili tofauti.

**WABUNGE FULANI:** Ahaa! (*Kicheko*)

Na. 6

**Walimu wa Kutosha Katika Shule Zetu**

**MHE. THOMAS NGAWAIYA** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali imefanya kazi kubwa sana ya kujenga Shule za Msingi na za Sekondari kwa gharama kubwa tu jambo la kuipongeza Serikali, lakini kuwa na nyumba/madarasa ya Shule bila kuwa na Walimu ni sawa na bure:-

(a) Je, Serikali imefanya jitihada gani za kuongeza idadi ya Walimu wanafunzi “trainers” kwa kuongeza Vyuo?

(b) Je, Serikali haioni kuwa kupeleka wanafunzi kwenda kujifunza katika nchi za India, China, Korea na kadhalika itaongeza tija na ufahamu mwingi kwa manufaa ya nchi yetu?

(c) Je, Serikali imeweka mazingira gani kuhakikisha kwamba, mipango ya Elimu ya *MMEM*, *MMES* na *MEMKWA* inakuwa endelevu na kujimudu hasa baada ya wafadhili kuondoka?

#### **WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Thomas Ngawaiya, Mbunge wa Moshi Vijijini, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza mpango wa *MMEM* (2002-2006) na *MMES* (2004-2009) Serikali imechukua hatua mbalimbali za kuongeza idadi ya Walimu wa Shule za Msingi na Sekondari ikiwa ni pamoja na :-

- Kuajiri Walimu wote wenye Vyeti vya Walimu waliofaulu mafunzo ya Ualimu miaka ya nyuma ambao walikuwa hawana ajira.
- Kuongeza nafasi katika Vyuo vya Ualimu vilivyopo ili kuchukua Walimu wanafunzi wengi zaidi.
- Kutoa mafunzo ya mwaka mmoja kwa Walimu wanafunzi ngazi ya Cheti na mwaka mmoja wa mazoezi.
- Kubadilisha Chuo cha Ualimu cha Dar es Salaam na Shule ya Sekondari ya Mkwawa kuwa Vyuo Vikuu Vishiriki vya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na Chuo cha Ualimu Mtwara kuwa Chuo Ambata cha Chuo Kikuu cha Dar es Salaam vitakavyotoa Elimu ya Ualimu kwa ajili ya Walimu wa Shule za Sekondari na Vyuo vya Ualimu.
- Kuajiri waliofaulu Kidato cha Sita na Wahitimu wa Chuo Kikuu wasio na Vyeti vya Ualimu ambao wanapatiwa mafunzo ya muda mfupi kuhusu mbinu za kufundishia.

(b) Mheshimiwa Spika, ni kweli kuwa kusomesha wanafunzi nje ya nchi kunaongeza tija na ufanisi katika utendaji kazi hapa nchini. Kwa muda mrefu tumekuwa tukipeleka wanafunzi na hata Walimu walioko kazini kusoma nchi za nje kwa lengo hilo,

ingawaje ni wanafunzi na Walimu wachache hupelekwa nchi za nje kutokana na ufinyu wa Bajeti.

(c) Mheshimiwa Spika, katika utekelezaji wa mpango wa *MMEM, MMES* na *MEMKWA*, Serikali imeweka mazingira mazuri ya aina mbili ya kuhakikisha kwamba mipango hii inakuwa endelevu hususani baada ya wafadhili kuondoka. Kwanza, mipango hii inatekelezwa kwa njia shirikishi, kwa kuwashirikisha wadau wote wa elimu. Kwa utaratibu huu, itakuwa rahisi kuendela na utekelezaji wa miradi hiyo hata mwisho wa mipango wakati wafadhili watakuwa wameondoka.

Pili, kutokana na ongezeko la kasi ya kukua kwa uchumi na ongezeko la mapato ya Serikali, gharama za uendeshaji wa miradi mbalimbali ikiwemo ya elimu itaweza kubebwa hapo baadaye na Bajeti ya Serikali kwa kuwa sehemu kubwa ya miundombinu itakuwa tayari imekwishawekwa.

**MHE. MAJOR JESSE J. MAKUNDI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza angalau swali moja la nyongeza. Kwa kuwa kumekuwa na neema ya kujengwa Shule za Sekondari karibu kila Kata na hivyo kuwapa nafuu wale waliofaulu kupata nafasi ya kuingia kwenye *Secondary Schools* hizo na hatimaye utakuta hakuna Walimu wa kutosha kufundisha katika Shule hizo:- Je, wale waliomaliza Kidato cha Sita wanaweza kupewa *crash programme* ambayo itawawezesha kwenda kufundisha kwenye hizo Sekondari?

Swali la pili; kwa kuwa *Form Six* au Kidato cha Sita wana fursa ya kwenda JKT na JKT kuna kozi mbalimbali za kiutaalamu na kiufundi na kadhalika:- Je, inawezekana huko JKT kuwe na somo la Ualimu ili hawa *Form Six* wakimaliza JKT waweze kwenda kushiriki kufundisha *Secondary School*? Ahsante.

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI:** Mheshimiwa Spika, sehemu ya (a) kuhusu *crash programme* kwa wale wa Kidato cha Sita, hili nililigusia katika jibu la msingi kwamba ni mkakati mmojawapo tunaoutumia pale ambapo tunajikuta tumeshindwa kuwapata Walimu ambao wamekwishapata mafunzo.

Mheshimiwa Spika, hatua ya kwanza tunayochukua ni kujaribu kuwapata Walimu wenye sifa za Ualimu zinazohitajika kufundisha katika Shule zetu za Sekondari. Ndani ya mfumo wa Shule wa Sekondari hivi sasa, wastani wa Mwalimu kwa wanafunzi, yaani *Pupil Teacher Ratio (PTR)* sasa hivi ni 1:23.

Kwa hiyo, upo uwezekano wa kuwaondoa Walimu kule ambako wamepangwa wa ziada na ndilo zoezi tunalolifanya kwanza kuwapeleka kwenye Shule hizi mpya zilizofunguliwa. Lakini napenda nikiri kwamba ufunguaji wa Shule za Sekondari mwaka huu, Shule mpya 386 ndani ya mwaka mmoja pamoja na kwamba ni mafanikio mazuri ya *take off* ya *SEDP*, lakini imezua tatizo kubwa la Walimu kuliko tulivyotegemea. Kwa hiyo, tuko katika mchakato wa kusawazisha kutoka kule kuliko na ziada kupeleka kuliko na upungufu. Tutakaporidhika kwamba sasa ipo *shortage* halisi ndipo tutatumia mkakati huu.

Mheshimiwa Spika, kwenye swali la (b) kwamba Kozi hizi zitolewe JKT, nina hakika Mheshimiwa *Major J.J. Makundi* anaelewa kwamba sehemu kubwa ya mambo yanayofanywa katika Kambi za JKT yamelalia zaidi kwenye mambo ya Kijeshi.

Sisi tunao utaratibu wetu wa Kozi fupi ambazo zitazingatia mbinu za ufundishaji mzuri yaani *pedagogue* hawa wanafunzi ambao tayari wana ujuzi wa masomo yale tunayowapangia kufundisha waliomaliza Kidato cha Sita, watapelele mafunzo mafupi ya *pedagogue* ili wakafundishe vizuri wakati tumewapangia kwamba nao baadaye waende kusomea *Diploma* za Ualimu.

## Na.7

### **Majengo ya *Masjid Nadua Yatumiwe* na Sekondari ya Kichangachui**

**MHE. DR. AMAN W. A. KABOUROU** aliuliza:-

Kwa kuwa wakazi wa Ujiji walikubali kuyatoa majengo yao waliyoyajenga kupitia Msikiti wa Masjid Nadua yatumike kama sehemu ya Shule ya Sekondari ya Kichangachui ili kuwasaidia wanafunzi wanaoshindwa kupata nafasi ya kungia Kidato cha Kwanza na kwa kuwa, Sekondari ya Kigoma iliyokuwa ikichukua wanafunzi wa masomo ya kutwa haifanyi hivyo sasa na kusababisha wanafunzi 160 kukosa nafasi za kuendelea na masomo:-

(a) Je, ni sababu gani zilizofanya Serikali isiyatumie majengo hayo ili wanafunzi wapate haki yao ya kusoma?

(b) Je, ni kweli kwamba, Serikali inaona ugumu wa kuyatumia majengo hayo kwa sababu za udini?

(c) Je, Serikali iko tayari kuifidia Halmashauri ya Mji wa Kigoma Ujiji Shilingi milioni nne zilizokwishatumika kwa ajili ya ukarabati wa majengo hayo?

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Amani Kabourou, Mbunge wa Kigoma Mjini, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, endapo taratibu za kukabidhi majengo hayo zitafuatwa na kukamilika, Serikali haitakuwa na sababu ya kutokuyatumia majengo hayo kuwa Shule ya Sekondari.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali katika utaoaji wa huduma hushirikiana na Taasisi mbalimbali zikiwemo za Dini. Zipo pia Shule nyingi za Msingi na Sekondari hapa nchini ambazo zilijengwa na Taasisi za Kidini ambazo sasa zinaendeshwa na Serikali.

Kwa hiyo, Serikali haina pingamizi lolote iwapo taratibu za kukabidhi kwa Serikali majengo yanayomilikiwa na Msikiti wa Masjid Nadua wa Mjini Kigoma Ujiji zitafuatwa.

(c) Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Shule za Sekondari za Kutwa zinajengwa na Wananchi wa sehemu husika kwa ushirikiano wa Halmashauri ya Wilaya/Manispaa/Mji au Jiji, kwa hiyo, hakuna sababu ya kutoa fidia kwa Halmashauri ya Mji wa Kigoma Ujiji ya Shilingi milioni nne zilizotumika kwa ajili ya ukarabati wa majengo hayo, kwa sababu yalikuwa ni maamuzi ya Halmashauri hiyo na wamiliki wa majengo hayo. Kwa hiyo, Halmashauri hiyo ilikuwa inatekeleza wajibu wake.

Katika mpango wa *MMES* 2004-2009 Serikali inatoa ruzuku ya maendeleo ya Shilingi milioni saba kwa darasa na Shilingi milioni tisa kwa nyumba ya Mwalimu ili kukamilisha ujenzi mpya wa madarasa na nyumba za Walimu.

Wingi wa madarasa unategemea nafasi mpya zinazohitajika katika kila Halmashauri ili kufikia lengo la kila mwaka la watahiniwa wa Darasa la Saba wa mwaka uliopita kupeleka Sekondari ambalo ni asilimia 35 mwaka 2005, 40 mwaka 2006, 45 mwaka 2007 na 50 mwaka 2008 na kuendelea kwa mpango wa *MMES* wa sasa.

Kwa utaratibu huo, madarasa yaliyoachiwa Sekondari ya Bweni ya Kigoma yatafidiwa mumo kwa mumo kupitia ruzuku ya maendeleo ambayo kwa mwaka huu peke yake imetolewa kwa Halmashauri ya Kigoma Ujiji jumla ya Shilingi Milioni 103, kwa ajili ya madarasa saba, milioni 49 na nyumba za walimu sita milioni 54. Kwa hiyo, ni zaidi hata ya ile milioni nne ambayo Mheshimiwa Kabourou alikuwa anaidai.

**MHE. DR. AMANI W.A. KABOUROU:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwa kuwa Mheshimiwa Waziri ameweza kujibu kwa ufasaha kiasi kwamba kwa kweli sina hoja zaidi:- Je, haoni kwamba Maafisa wake wa Elimu walioko kule Kigoma wanamwangusha kwa kushindwa kuwafafanulia wananchi masuala kama alivyofafanua Waziri mwenyewe, haoni kwamba Maafisa wake wanamwangusha?

**SPIKA:** Lakini watakuwa wamesikia majibu ya Mheshimiwa Waziri. Endelea kujibu.

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI:** Mheshimiwa Spika, naomba kumjibu Mheshimiwa Mbunge swali lake la nyongeza kama ifuatavyo:- Mimi silioni suala lolote la Maafisa Elimu kuniangusha kwa sababu wanayo maelekezo haya, isipokuwa Mheshimiwa Mbunge ni sehemu ya wajibu wake kwamba Mawaziri tukifafanua mambo hapa naye anakwenda kusaidia kufafanua kule. Hii ndio itasaidia zaidi. *(Makofi)*



Na. 8

### **Takrima**

**MHE. LEONARD M. SHANGO (k.n.y. MHE. MGANA I. MSINDAI)**

Aliuliza:-

Kwa kuwa, Sheria inayoruhusu Takrima kutumika wakati wa shughuli zote za kisiasa na wakati wa Kampeni za Uchaguzi inapingwa kwa nguvu zote na watu wengi yakiwemo Mashirika mbalimbali ya ndani na nje na hata wananchi katika Vyama vya Siasa na kwa kuwa Serikali inakubali bado takrima iendelee kutumika hapo Mgombea anapokuwa na watu wanaomsaidia kwa kuwapa vifaa, chakula na vinywaji kwa sababu wapo kazini:-

(a) Je, kwa nini Serikali isikubali matakwa ya wengi kwamba, sheria hiyo ifanyiwe mabadiliko na kufanya kitu kinachojulikana kama gharama za uchaguzi na Serikali itenge fungu maalum kwa ajili ya Wagombea wote bila kujali itikadi zao za kisiasa?

(b) Je, Serikali haioni kuwa kuendelea kuikumbatia Takrima kunaivunja nchi yetu heshima ambayo imejijengea ndani na nje ya nchi?

(c) Kwa kuwa, Madiwani, Wabunge na Mheshimiwa Rais wa nchi walioko madarakani sasa kuna mambo waliyotolea ahadi wapigakura wao kwamba watafanya katika kipindi chao cha uongozi mambo mbali mbali kama ujenzi wa barabara, maji, afya, elimu, mawasiliano, vifaa vya michezo mashuleni, Vitabu na kadhalika, kuimarisha Vyama vyao kwa kutoa kadi, bendera, sare, vyombo vya usafiri na kadhalika na wahusika walianza kutoa vitu hivi tangu walipochaguliwa:- Je, kwa nini kwa baadhi ya maeneo wahusika wakitoa ahadi hizo wanasumbuliwa na kuambiwa wanatoa rushwa/wanahonga mali zao na bado kwenye kipindi cha ahadi walizotoa kwa wananchi wa maeneo hayo?

**WAZIRI WA SHERIA NA MAMBO YA KATIBA alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, ningependa kujibu swali la Mheshimiwa Mgana Msindai, Mbunge wa Iramba Mashariki, lenye sehemu (a), (b) na (c) kwa pamoja, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, awali ya yote naomba nieleze wazi kuwa Serikali inapiga vita rushwa na kwa maana hiyo mkakati wa Taifa wa kupambana nayo unaendelea kutekelezwa na Serikali ya Awamu ya Tatu kwa nguvu zake zote.

Katika eneo la Uchaguzi, Sheria ya Uchaguzi Na.1 ya mwaka 1985 inaziendeleza jitihada hizo. Sheria inaainisha vitendo mbalimbali ambavyo endapo vitafanyika, vitahesabika moja kwa moja kuwa ni vitendo vya rushwa na sheria imeweka adhabu kali kwa vitendo hivyo. Fungu la 97(1) la sheria hiyo linaainisha na kufafanua vitendo

mbalimbali vinavyohesabika kuwa ni rushwa katika Uchaguzi hususan vile vitendo vinavyohusu matumizi ya fedha au vitu vingine vyenye thamani kabla au wakati wa kampeni kwa nia ya kuwashawishi watu wapige au kutopiga kura au kwa nia ya kuathiri matokeo ya uchaguzi.

Fungu la 97(2) na (4) linafafanua wazi kuwa pale mtu anapolipa au kulipwa fedha kwa ajili ya gharama zilizofikiwa kihalali na kwa nia njema kuhusiana na uchaguzi, siyo rushwa.

Aidha, kitendo hakitahesabiwa kuwa ni rushwa kama kimefanywa kwa ajili ya kuendeleza maslahi ya Umma kwa maana ya kupata fedha za kutekeleza mipango ya Ustawi wa jamii au kwa maana ya kujitolea au kujitegemea iwapo vitendo kama hivyo vimefanyika kabla ya muda wa kampeni.

Mheshimiwa Spika, kuhusu vitendo vya ukarimu, fungu la 98(1) la Sheria ya Uchaguzi linaainisha wazi kuwa, vitendo vya ukarimu kwa maana ya kutoa vyakula, vinywaji, burudani au huduma nyingine kwa nia ya kuathiri matokeo ya uchaguzi kwa kufanya watu wapige au waache kupiga kura, vitahesabika kuwa ni vitendo vya rushwa.

Hata hivyo, Kifungu cha 98(2) na (3), kinaainisha wazi kuwa vitendo vya takrima ambavyo hufanywa kwa nia njema kama vitendo vya ukarimu wa kimila (*traditional hospitality*) ikiwa ni pamoja na gharama za ukarimu wa kawaida wakati wa kampeni, havitahesabika kuwa ni vitendo vya rushwa. Kwa maana hiyo ule ukarimu unaofanywa katika misingi ya asili na mila zetu, siyo rushwa.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia mazingira ya kila sheria, Mahakama ndiyo yenye jukumu la kuamua kama kitendo kilichofanyika ni cha rushwa au ni cha ukarimu wa kawaida katika jamii inayohusika. Serikali inaamini kuwa Mahakama itaweza kuweka bayana kati ya matendo ya rushwa na yale matendo ambayo ni ya ukarimu wa kawaida katika mila zetu.

Mheshimiwa Spika, hivi sasa ipo kesi Mahakamani kuhusu suala hili. Naomba nisiingie ndani zaidi ya kuelezea kile tu ambacho sheria yenyewe inasema. Aidha, napenda nieleze Bunge lako Tukufu kwamba, utekelezaji wa ahadi zilizotolewa wakati wa Kampeni ya Uchaguzi uliopita pamoja na utekelezaji wa ahadi zilizotolewa katika Ilani za Vyama vya Siasa, siyo rushwa. Kimsingi siyo nia ya sheria au taratibu zetu, kudumaza maendeleo wakati wa uchaguzi.

**MHE. LEONARD M. SHANGO:** Mheshimiwa Spika, asante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, nina swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa suala la Takrima kama wengi wanavyolielewa halina mipaka:- Je, Serikali inaweza kutoa kauli au maelekezo kuhusu vitendo vinavyoendelea sasa vya Wagombea watarajiwa wa Vyama mbalimbali kusambaza kwa wananchi zawadi za kila aina wakati Taifa linaelekea kwenye Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2005?

**SPIKA:** Sawa tumesikia, Mheshimiwa Waziri majibu!

**WAZIRI WA SHERIA NA MAMBO YA KATIBA:** Mheshimiwa Spika, nadhani kama tukisoma sheria yenyewe, tunaweza tukaelewa vizuri suala lenyewe, Sheria imebainisha kabisa na iko wazi katika masuala hayo. Yapi?! Kama nilivyozungumza katika jibu langu la msingi maeneo ambayo yanaendana na masuala ya rushwa na yale ambayo siyo ya rushwa. Mathalani, Kifungu 98(2), kinasema hivi:- *For the purposes of section one, anything done in good faith as an act of normal traditional hospitality, shall be deemed not to be treaty. (3) No more ordinary expenses spent in good faith, in the election campaign or the ordinary course of election process, shall be deemed not to be treating, bribery or illegal practice.*” Sasa haya ni masuala ambayo yakijitokeza, basi Mahakama ndiyo yenye mamlaka ya mwisho kuweza kuyafafanua.

**MHE. ISAAC M. CHEYO:** Mheshimiwa Spika, kitendo cha nia njema, nilikuwa nategemea kwamba kingekuwapo hata tangu mwanzo kabla ya wakati wa uchaguzi.

Lakini kitendo cha nia njema kinapokuwa tu ni wakati wa uchaguzi, watu wanatoa *in advance*, kutoa baiskeli, kutoa vyakula mapema kwa lengo la kutaka kushawishi kuchaguliwa:- Je, Waziri halioni hilo kama ni mwanzo kabisa wa rushwa na hivi lilikuwa linatakiwa kukemewa na kufutwa moja kwa moja watu wa namna hiyo?

**WAZIRI WA SHERIA NA MAMBO YA KATIBA:** Mheshimiwa Spika, mimi ni mmojawapo ambaye nikiwa kama ni Mbunge wa Chama Cha Mapinduzi katika Jimbo langu la Tanga, nimetoa baiskeli, nimetoa vyerehani, kwa maana ya kukiwezesha Chama changu kuendeleza shughuli zake. Sikumpa mtu binafsi, nimetoa zile baiskeli na vifaa vingine kwa Chama. Kwa hiyo, hata wewe nadhani umeshatoa huko. (*Kicheko/Makofi*)

**MHE. PHILIP S. MARMO:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. (*Kicheko*)

Pamoja na majibu mazuri na ya kina ya Waziri, bado kuna utata katika suala hili la Takrima. Je, Waziri haoni kwamba sasa wakati umefika, sababu jambo hili linaleta ubishani, sasa tuweke bayana, nini gharama hasa ya uchaguzi. Kwa sababu uchaguzi una gharama. Kwa nini sheria isitaje gharama ya uchaguzi na kiwango chake cha juu?

Pili, pia sheria itaje, mchango wa Mwanasiasa kwa jamii na muda katika miaka mitano ambayo shughuli za mwakilishi zinaendelea. Ahsante.

**WAZIRI WA SHERIA NA MAMBO YA KATIBA:** Mheshimiwa Spika, labda kisera ni kweli. *I mean* suala hili limekuwa likitolewa hoja na watu mbalimbali, Waheshimiwa Wabunge, Viongozi wa Dini na watu wengine.

Kutokana na hoja hizi, basi, Mwanasheria Mkuu wa Serikali, ameliwasilisha suala hili kwenye Tume ya Kurekebisha Sheria na kama unavyojua Mheshimiwa Spika na wewe ni Mjumbe, Mheshimiwa Asha-Rose ni Mjumbe, wamekwishatayarisha ripoti

ambayo mimi nimekabidhiwa na tunaifanyia kazi ili kuweza kufafanua masuala yote haya.

Na. 9

### **Tatizo la Usafiri kwa Wanafunzi Katika Miji Nchini**

**MHE. USSI YAHAYA HAJI** aliuliza:

Kwa kuwa , wanafunzi hususan katika Jiji la Dar es salaam, wamekuwa wakipata tabu na kusumbuliwa na wenye mabasi ya usafiri Jijini hapo na kwa kuwa Serikali imejitahidi sana kwa muda mrefu kuboresha usafiri wa wanafunzi katika Miji Mikuu kama vile Dar es salaam, Arusha, Mwanza, Morogoro na kadhalika bila mafanikio:-

(a) Je, Serikali haioni kwamba wakati umefika sasa wa kutafuta ufumbuzi wa kudumu wanafunzi wa Mjini kwa kuwapatia usafiri; hususan katika Jiji la Dar es salaam ambapo wanateseka na kunyanyasika sana?

(b) Je, Serikali inasema nini kuhusiana na kuwataka Wawekezaji kuwekeza katika usafiri hususan kwa mabasi ya wanafunzi katika Miji Mikuu ili kuliondoa kabisa tatizo hilo?

(d) Iwapo watajitokeza Wawekezaji hao:- Je, Serikali iko tayari kuwasamehe baadhi ya kodi kwa kuwekeza katika usafiri wa wanafunzi?

**WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI** alijibu:-

Haijapata kutokea! (*Kicheko na Makofi*)

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ussi Yahaya Haji, Mbunge wa Chaani kama ifuatavyo:-

Nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa tatizo la wanafunzi kunyanyaswa na makondakta wa Mabasi ya Daladala bado lipo na linaendelea. Wanafunzi wananyanyaswa kwa sababu nyingi lakini kubwa zaidi ni nauli ndogo wanayolipa ambayo wasafirishaji wa Daladala wanaona wanapata hasara.

Serikali kupitia Mamlaka ya Usafirishaji Mijini, imebuni Mradi wa Mabasi yaendayo kasi. Hatua zote za awali tayari zimechukuliwa na tunategemea Mradi huu utakapoanza, utaboresha kwa kiasi kikubwa usafiri katika Jiji la Dar es salaam na hivyo kupunguza tatizo la uchukuzi kwa wanafunzi.

Mheshimiwa Spika, napenda nichukue fursa hii kuwapongeza Viongozi wa Shule mbalimbali waliobuni na hatimaye kuanzisha huduma za usafiri kwa wanafunzi wao katika Shule zao. Pia natoa wito kwa Shule nyingine ziige mfano. Naamini kwa kufanya

hivyo tutapunguza kwa kiasi kikubwa matatizo ya usafiri Mijini. Serikali kwa upande wake itaendelea kuwahamasisha wawekezaji kuwekeza katika Miradi ya Usafiri Mijini ili kupunguza matatizo ya usafiri.

Mheshimiwa Spika, ili kupunguza tatizo la usafiri wa wanafunzi Dar es salaam na katika Miji mingine, Wizara ya Elimu na Utamaduni imeshauri Halmashauri husika ziwaandikishe wanafunzi wapya katika Kata zao.

Mheshimiwa Spika, kutokana na mageuzi ya kiuchumi, Serikali imejitoa katika shughuli za kibiashara. Serikali haina uwezo wa kutoa ruzuku kwa sasa.

Mheshimiwa Spika, kwa kuuliza swali linalohusu tatizo la usafiri wa wanafunzi katika Jiji la Dar es salaam, Mheshimiwa Ussi Yahaya Haji anatumkumbusha kwamba tatizo hili linahusu Miji mingine mikubwa nchini kama vile Mwanza, Arusha, Mbeya, Iringa na Tanga. Anatumkumbusha vile vile changamoto kubwa ya kuwezesha usafiri wa wanafunzi katika maeneo ya Vijijini hasa kutokana na mafanikio ya mipango ya kuboresha Elimu ya Msingi na Elimu ya Sekondari.

Mheshimiwa Spika, tunatambua mchango mkubwa aliutoa Mheshimiwa Ussi Yahaya Haji kwa Sekta ya Uchukuzi nchini na katika maendeleo ya Jimbo la Chaani, tunamshukuru.

**MHE. ATHUMANI S.M. JANGUO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi kuuliza swali la nyongeza. Kuhusu mabasi yanayokwenda kasi Dar es salaam ambayo Mheshimiwa Waziri anategemea kuyaleta, tukizingatia kwamba Dar es salaam, magari ni mengi sana na barabara ni nyembamba mno:- Je, anakubaliana nami kwamba mabasi haya hayatakwenda kasi na kwamba wanafunzi watakuwa wanachelewa kwenda Shuleni? (*Makofi*)

**WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Spika, Kwanza kabisa sifa zote za mabasi yatakayokwenda kasi Dar es salaam, ni za Halmashauri ya Jiji la Dar es salaam wala si za Wizara ya Mawasiliano. Kwa hiyo, tunawashukuru kwa kuibua na kubuni na kufikiria huo mradi ambao utakuwa na manufaa kwa wakazi wa Jiji la Dar es salaam.

Pili, ni kwamba hivi sasa kuna Mtaalam Mwelekezi ambaye kazi yake ni kufanya utafiti, lakini kubuni mpango ambao utafanikisha kutenga barabara fulani Dar es salaam ambazo magari yatakayokwenda kasi yatakuwa yanapita. Kwa hivyo, akimaliza ripoti yake ambayo itatumika katika utekelezaji wa mradi huu, nina hakika utafanikisha sana uchukuzi Dar es salaam pamoja na uchukuzi wa wanafunzi katika Jiji la Dar es salaam.

**SPIKA:** Wakati wa Mkutano wa Bajeti, maswali humalizika saa nne, lakini leo hatukuanza saa tatu. Tulichelewa kuanza maswali. Kwa hiyo kuna muda wa kumaliza swali lililobaki la Mheshimiwa Mossy Mussa. Yeye hayupo, Muulizie swali lake, Mheshimiwa wa Kiwani.

**Na. 10**

**Hasara Iliyotokana na Ajali ya Treni Mwaka 2002**

**MHE. ZUHURA SHAMIS ABDALLAH (k.n.y. MHE. MOSSY SULEIMAN MUSSA) aliuliza:-**

Kwa kuwa mwaka 2002 nchi yetu ilikumbwa na msiba mkubwa uliotuachia majonzi makali kutokana na vifo vya Watanzania wenzetu vilivyosababishwa na ajali mbaya ya treni, ambayo licha ya kupata hasara ya kupoteza Watanzania wenzetu, pia tumepata hasara ya mali na vifaa mbali mbali vilivyopotea wakati wa tukio hilo:-

(a) Je, Serikali ilipata hasara kiasi gani kutokana na kuharibika kwa mabehewa ya treni hiyo?

(b) Je, ni mabehewa mangapi yaliyoweza kutengenezeka na kwa gharama gani?

**WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mossy Suleiman Mussa, Mbunge wa Mfenesini lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Serikali ilipata hasara ya Dola za Kimarekani 4,290,000. sawa na Shilingi 4,582,000,000/= kutokana na kuharibika kwa mabehewa 12, yakiwemo moja la daraja la kwanza, moja la daraja la pili na nane ya daraja la tatu, moja la Mgahawa na moja la vifurushi.

(b) Mheshimiwa Spika, Mabehewa yaliyoweza kutengenezwa ni 10 kwa gharama za Euro 675,000. zilizotolewa na Serikali ya Ujerumani, tunawashukuru.

Mheshimiwa Spika, hasara zaidi tuliyoipata kama Taifa ni kuwapoteza ndugu zetu, wajenzi wa Taifa letu. Pengo hilo haliwezi kuzibika kwa gharama yoyote ile.

Mheshimiwa Spika, Wizara kupitia Shirika la Reli Tanzania, inajitahidi kuboresha miuondombinu ya reli, kukarabati njia, kuamsha ari ya wafanyakazi wake kwa lengo la kuongeza ufanisi na kubwa zaidi kutambua umuhimu wa kusimamia usalama wa usafiri wa reli.

Mheshimiwa Spika tunamshukuru Mheshimiwa Mossy Suleiman Mussa Mbunge wa Mfenesini kwa kuendelea kutukumbusha kuhusu masuala haya ya muhimu katika sekta ya Uchukuzi.

**SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, maswali yamekwisha na muda wa maswali umekwisha na sasa kabla hatujasoma Muswada huu kwa mara ya kwanza tu siyo hatua zake zote lakini mara ya kwanza peke yake, ni matangazo ya Vikao kama nilivyokwishatamka mapema.

Kamati ya Sheria, Katiba na Utawala pamoja na Tume ya Huduma za Bunge tunakutana kwa pamoja katika chumba cha Mikutano cha Spika, ghorofa ya pili.

Halafu, nimeambiwa na Mwenyekiti wa Kamati ya Wabunge wote wa CCM kwamba kutakuwa na Kikao saa 11.00 jioni leo katika Ukumbi huu. Mwisho wa Matangazo.

## **MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI**

*(Kusomwa Mara ya Kwanza)*

**Muswada wa Sheria ya kurekebisha sheria mbalimbali wa Mwaka 2005 (*The Written Laws(Miscellaneous Amendments) (No. 2) Bill,2005*)**

*(Muswada uliotajwa hapo juu, ulisomwa Bungeni kwa mara ya kwanza)*

**SPIKA:** Muswada huo umesomwa kwa mara ya kwanza. Sasa utaendelea na hatua zake katika Kamati. Kwa sababu hatuna kazi ya kufanya tena kwa siku ya leo, sasa naihirisha Kikao hiki cha Bunge hadi kesho saa tatu.

*(Saa 04.07 Asubuhi Bunge lililahirishwa Mpaka Siku ya Jumatano  
Tarehe 08 Juni, 2005 Saa Tatu Asubuhi)*